



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA



**TANGAZO LA USAJILI WA WATAALAMU ELEKEZI WA MAZINGIRA KUPITIA
MFUMO WA KIELEKTONIKI**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepewa dhamana ya kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) pamoja na usajili na usimamizi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Aidha, Ibara ya 83 ya Sheria ya Mazingira imeanisha kuwa TAM itafanywa na Mtaalam Elekezi wa Mazingira ambaye jina lake pamoja na taaluma vimesajiliwa na Baraza.

Hivyo, katika kuboresha mifumo yake na huduma kwa wadau, Baraza limeboresha mfumo wa kielektroniki wa kusajili Miradi ya Tathmini za Mazingira na Ukaguzi (*Online Registration and Tracking System*) kwa kuongeza kipengele cha usajili wa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Maboresho hayo yatawezesha wote wenye sifa za kuwa Wataalam Elekezi wa Mazingira kuwasilisha maombi yao ya usajili na utendaji (Registration and Practice) kwa mujibu wa Kanuni za Usajili na Utendaji wa Wataalam Elekezi za mwaka 2021 (Environmental Management (Registration and Practice of Environmental Experts) regulations, 2021). Vile vile, mfumo huo utawezesha Wataalam Elekezi kufanyia kazi miradi ya TAM katika akaunti zao wenyewe.

Mfumo huu unapatikana kwenye tovuti ya Baraza kupitia eia.nemc.or.tz

Kufuatia maboresho hayo, Baraza linawaatarifu kuwa maombi yote ya Cheti cha Usajili na Cheti cha Utendaji wa Utaalam Elekezi wa Mazingira (*Environmental Experts Registration Certificate and Environmental Experts Practicing Certificate*) yafanyike kupitia mfumo wa kielektroniki. **Baraza halitapokea maombi mapya kwa njia ya kawaida kuanzia tarehe 1 Julai 2022.**

Kwa msaada zaidi unaweza kuwasiliana nasi kwa kupitia eiasupport@nemc.or.tz au tovuti ya Baraza (nemc.or.tz) au tembelea Ofisi za Makao Makuu ya Baraza zilizopo katika kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent, Mikocheni au katika ofisi za kanda za Baraza zilizopo Arusha, Dodoma, Mbeya, Kigoma, Morogoro, Mwanza na Mtwara.

Tangazo hili limetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira,
Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent Mikocheni,
S.L.P 63154
Dar es Salaam.

Simu ya mezani: +255 22 277 4889, moja kwa moja +255 22 277 4852

Simu ya mkononi: 0713 606930/0692 108566

Fax: +255 222774901

Barua pepe: dg@nemc.or.tz